

## **HABARI MUHIMU KUHUSU MANUFAA YA BIMA YAKO YA MEDICAID.**

### **Tafadhali Chukua Hatua Mara Moja**

Tunaandika ili kukupa habari muhimu kuhusu manufaa ya bima yako ya Medicaid. Kama inavyohitajika na sheria ya nchi, Jimbo la Rhode Island linatekeleza shughuli ya usasishaji wa ustahiki wa bima ya Medicaid ili kuthibitisha kwamba kila mtu anayepokea bima ya Medicaid anaendelea kustahiki. Rekodi zetu zinaonyesha kwamba una hali maalum zinazoathiri ustahiki wako.

#### **Muda wa matumizi ya Bima yako ya Medicaid Unaisha**

Maeleo tuliyo nayo yanaonyesha kwamba hustahiki kupokea bima ya Medicaid kwa sababu ya hali yako ya uhamiaji. Tumejaribu kuhakikisha hali yako ya uhamiaji kuitia vyanzo vilivyopo tunavyoweza kuvipata, lakini tumeshindwa kuthibitisha hali yako. Hatuna hati tunazohitaji ili kuthibitisha ikiwa unastahiki kuendelea kupokea huduma ya bima.

#### **Jinsi ya Kutambua Ikiwa Unaweza Kuendelea Kupokea Bima ya Medicaid**

Ikiwa ungependa kuendelea kupokea huduma ya bima ya Medicaid, tafadhali wasilisha hati tunazohitaji ili kuthibitisha ustahiki wako wa kupokea bima ya Medicaid. Unaweza kupata maeleo zaidi kuhusu hati tunazohitaji kwa:

- Kuingia kwenye akaunti yako katika [www.healthyrhode.ri.gov](http://www.healthyrhode.ri.gov). Ukurasa wa "My Dashboard" (Dashibodi Yangu) utaonyesha hati ambazo ni lazima uwasilishe.
- Kuwasiliana na Idara ya Huduma za Binadamu (Department of Human Services, DHS) ya Rhode Island kwa nambari 1-855-697-4347.

Usichelewe. Tafadhali kagua hati zako na uwasilishe maelezo yaliyosasishwa mara moja ili tuweze kuthibitisha ikiwa unastahiki kuendelea kupokea huduma ya bima.

**Unachoweza Kufanya Ikiwa Hustahiki Tena Kupokea Bima ya Medicaid**

Ikiwa wewe ni mkazi halali nchini Marekani na unatimiza masharti ya ustahiki wa hali ya uhamiaji, unaweza kuwa na chaguo zingine za kuendelea kupokea huduma ya bima kuitia HealthSource RI (HSRI). Wasiliana na HSRI kuanzia saa 8 a.m. hadi 6 p.m. siku za wiki kwa nambari 1-855-840-4774 ili uzungumze na mtu anayeweza kukusaidia.

Ikiwa hukubali uamuzi wetu kuhusu manufaa yako, unaweza kukata rufaa kwa kufuata utaratibu ulioelezwa kwenye Notisi ya Uamuzi wa Manufaa yako (Benefit Decision Notice).

Tembelea [www.staycovered.ri.gov](http://www.staycovered.ri.gov) ili upate maelezo zaidi kuhusu ustahiki wa kupokea bima ya Medicaid na jinsi ya kuomba msaada.